# K.J.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA JUNIA
# TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 2, 2026
# GREDI YA 7 – KISWAHILI
# Muda: Saa 1 Dakika 40

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: _____ Shule: _____

Nambari ya Tathmini: _____ Tarehe: _____

Nambari ya Shule: _____ Sahihi: _____

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.

JEDWALI LA ALAMA

| SEHEMU | SEHEMU A | SEHEMU B | SEHEMU C | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 25 | ALAMA 10 | ALAMA 15 | | 90–100 | 75–89 | 58–74 | 41–57 | 31–40 | 21–30 | 11–20 | 1–10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 9.**

Jiji la Mwanga, lililopo kaskazini mwa nchi, limekuwa mfano bora wa kuigwa katika kudumisha usalama wa wakazi wake. Chini ya uongozi wa Kamishna Sofia Kazi, mifumo ya usalama imeimarishwa kwa kuwekwa kamera za ulinzi (CCTV) na kuboreshwa kwa huduma za dharura. Aidha, polisi wameimarisha ushirikiano wao na jamii kwa karibu zaidi.

Katika soko la Kitema, Omari, ambaye ni mfanyabiashara mdogo, anathibitisha kuwa hali ya usalama imeboreshwa sana. Anaeleza kuwa kwa sasa watu wanaweza kuendesha shughuli zao za kila siku bila hofu kubwa.

Vilevile, mpango wa “Jirani Mlinzi” umeanzishwa ambapo wananchi hushiriki kikamilifu katika doria na kutoa taarifa kuhusu vitendo vya uhalifu. Pia, kuna vituo maalum vinavyotoa msaada kwa wanawake na watoto wanaokumbwa na ukatili, vikitoa huduma za kisheria na ushauri wa kisaikolojia.

Kupitia juhudi hizi za pamoja, jiji la Mwanga halijaendelea tu kiuchumi bali pia limejijengea sifa nzuri kama jiji lenye amani, mshikamano na usalama wa hali ya juu.

1. Ni hatua ipi kuu iliyochukuliwa na Kamishna Sofia Kazi kuboresha usalama?
   A. Kuwafukuza wahalifu wote
   B. Kujenga shule za polisi
   C. Kuweka kamera za ulinzi na kushirikisha jamii
   D. Kuzuia watu kuingia jijini
2. Kwa nini Omari anaamini usalama umeimarika?
   A. Ameajiriwa serikalini
   B. Biashara zinafungwa mapema
   C. Watu wanafanya shughuli zao bila hofu
   D. Ana mlinzi binafsi
3. Mpango wa “Jirani Mlinzi” unalenga nini?
   A. Kuwapa vijana ajira
   B. Kushirikisha jamii katika kulinda usalama
   C. Kuwazuia wazee kushiriki
   D. Kujenga vituo vya polisi
4. Ni huduma gani hutolewa kwa wanawake na watoto?
   A. Vituo vya michezo
   B. Msaada wa kisheria na ushauri
   C. Maeneo ya biashara
   D. Mafunzo ya ujasiriamali
5. Polisi wanashirikiana vipi na wananchi?
   A. Kuwapa mafunzo ya kijeshi
   B. Kufanya mikutano sokoni
   C. Kutumia teknolojia na miradi ya kijamii
   D. Kufanya kazi za soko
6. Kwa mujibu wa kifungu, usalama wa jiji la Mwanga umeimarika kutokana na nini?
   A. Kuongezeka kwa askari wengi
   B. Ushirikiano kati ya polisi na jamii
   C. Kufungwa kwa biashara
   D. Uhamiaji wa watu
7. Ni ipi kauli sahihi kuhusu jiji la Mwanga?
   A. Limejaa uhalifu
   B. Linahitaji msaada wa nje
   C. Lina amani na maendeleo
   D. Halijaendelea
8. Kwa nini watoto wanalindwa zaidi?
   A. Huchelewa shule
   B. Hucheza sana mitaani
   C. Ili kuwalinda dhidi ya hatari na ukatili
   D. Wanahitaji ajira
9. Usalama unafanikiwa vipi kulingana na kifungu?
   A. Walinzi wengi kila mahali
   B. Adhabu kali kwa wahalifu
   C. Kujenga barabara
   D. Ushirikiano wa serikali, polisi na wananchi
10. Ni faida gani kuu ya juhudi hizi kwa jiji la Mwanga?
    A. Kupungua kwa watu
    B. Kuongezeka kwa ushuru
    C. Kuimarika kwa uchumi na amani
    D. Kufungwa kwa soko

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 10 hadi 17.**

Kijiji cha Mwangaza, kilichopo nyanda za Kivulini, kilikuwa kikitegemea kuni na makaa kwa matumizi ya kila siku. Hali hiyo ilisababisha ukataji miti ovyo, moshi majumbani, na matatizo ya kiafya hasa kwa wanawake na watoto.

Mama Halima, mkulima na mjasiriamali wa kijiji hicho, aliona haja ya mabadiliko. Kwa kushirikiana na Kassim, mwanafunzi wa uhandisi aliyekuwa likizo, walihamasisha matumizi ya nishati safi kama vile majiko ya gesi na sola.

Mama Halima aliandaa warsha na mikutano ya akina mama, huku Kassim akieleza kwa vitendo jinsi ya kutumia paneli za sola na majiko ya kisasa kwa gharama nafuu. Walitafuta wafadhili waliosaidia kutoa vifaa vya mwanzo kwa familia kadhaa.

Kwa msaada wa serikali ya kata na mashirika ya mazingira, nishati safi ilianza kutumika katika nyumba nyingi. Sauti za kuni zikavurugika na moshi ukapungua. Wanawake walipata muda zaidi wa kujihusisha na shughuli za maendeleo, watoto wakasoma bila shida usiku, na mazingira yakaanza kurejea katika hali ya asili. Mwangaza ukawa si jina tu la kijiji, bali ishara ya maendeleo kupitia nishati bora na mshikamano wa jamii.

10. Ni changamoto gani kuu iliyokuwa ikikikabili Kijiji cha Mwangaza?
    A. Ukosefu wa shule.
    B. Ukosefu wa hospitali.
    C. Kutegemea kuni na mkaa kwa matumizi ya kila siku.
    D. Ukosefu wa barabara.
11. Ni nani aliyetajwa kuchukua hatua za kuboresha matumizi ya nishati katika kijiji hicho?
    A. Mama Halima na Kassim.
    B. Wanafunzi wa uhandisi.
    C. Mwalimu mkuu.
    D. Serikali ya kata.

12. Kassim alichangiaje katika juhudi za kuboresha nishati kijijini?
    A. Alitoa mikutano kwa wanawake.
    B. Alieleza jinsi ya kutumia paneli za sola na majiko ya gesi.
    C. Alitafuta wafadhili wa majengo ya shule.
    D. Alitangaza miradi ya maendeleo kwenye redio.
13. Ni faida gani kuu zilizotokana na matumizi ya nishati safi katika kijiji cha Mwangaza?
    A. Kupungua kwa moshi na ukataji miti ovyo.
    B. Kuongezeka kwa gharama za maisha.
    C. Kupungua kwa michezo mitaani.
    D. Kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira.
14. Mama Halima alihamasisha kundi gani kuhusu matumizi ya nishati safi?
    A. Vijana wa kijiji.
    B. Akina mama.
    C. Wazee wa kijiji.
    D. Wanafunzi wa shule.
15. Ni msaada gani uliochangia upatikanaji wa vifaa vya nishati safi kwa familia?
    A. Misaada ya serikali ya kata na mashirika ya mazingira.
    B. Misaada kutoka kwa wafadhili wa miji mingine.
    C. Mikopo kutoka benki.
    D. Misaada ya chakula.
16. Kwa mujibu wa kifungu, nishati safi iliathirije maisha ya wanawake na watoto?
    A. Kuwasaidia kupata kazi mpya.
    B. Kuwapatia muda zaidi kwa shughuli za maendeleo na kusoma usiku.
    C. Kuwapa chakula bora.
    D. Kuwalinda dhidi ya magonjwa ya ngozi.
17. Kijiji cha Mwangaza kilipata sifa gani baada ya kutumia nishati safi? Kilikuwa
    A. kijiji kilichojaa uchafu
    B. ishara ya maendeleo na mshikamano wa jamii
    C. eneo la kutotembelewa na wageni
    D. kijiji cha maskini zaidi.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 18 hadi la 20.**

Bwana Juma anamiliki shamba kubwa la matunda. Ana aina tano za matunda anayouza sokoni: maembe, machungwa, ndizi, maparachichi na papai. Ana wateja wanne wakuu: Zawadi, Baraka, Neema na Imani. Kila mteja ananunua matunda tofauti kila siku za wiki kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Tazama jedwali lifuatalo:

| **Siku** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mteja** | | | | | |
| Zawadi | Maembe | Ndizi | Machungwa | Papai | Maparachichi |
| Baraka | Ndizi | Maembe | Papai | Maembe | Machungwa |
| Neema | Papai | Machungwa | Maembe | Ndizi | Papai |
| Imani | Papai | Machungwa | Ndizi | Maembe | Machungwa |

18. Chagua jibu lenye jina la mteja ambaye hununua aina moja tu ya tunda mara tatu kwa wiki.
    A. Zawadi
    B. Baraka
    C. Neema
    D. Imani
19. Matunda gani yanauzwa kwa wingi siku ya Ijumaa?
    A. Papai
    B. Machungwa
    C. Maembe
    D. Maparachichi
20. Chagua jibu lenye siku ambayo kila mteja wa Bwana Juma hununua tunda linalotofautiana na la wenzake.
    A. Jumatatu
    B. Jumanne
    C. Jumatano
    D. Alhamisi

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 21 hadi la 25.**

*(Ni jioni. Mama Pendo amekaa nje ya nyumba yake akisoma gazeti. Mtoto wake, Neema, anakuja mbio akitoka shuleni.)*

**Neema:** (Akinaswa na pumzi.) Mama, mama! Nimekuja!

**Mama Pendo:** (Akiinua macho yake kutoka gazetini, akitabasamu.) Karibu mwanangu. **21. …..** umefika salama?
**Neema:** Ndiyo mama, nimefika salama. Leo kulikuwa na mambo mengi shuleni.

**Mama Pendo:** (Kwa upole.) Haya, nambia. Nini kilitokea?

**Neema:** Tulikuwa na mgeni mwalimu wa Kiswahili. Alitufundisha mada mpya ya methali. Alisema methali ni **22. hazina** za jamii.

**Mama Pendo:** Ah, kweli kabisa! Methali zina hekima kubwa. Ni muhimu kuzielewa.

**Neema:** Ndiyo mama. Lakini kuna methali moja iliniacha na maswali mengi. "Mpanda ovyo hula ovyo." Sijaielewa vyema.

**Mama Pendo:** (Akifikiri kwa muda mfupi.) Maana yake ni rahisi, Neema. Ina maana kwamba, **23. …..**Mtu asiyejiandaa vizuri hawezi kutarajia mafanikio.

**Neema:** *(Akinyenyekea.)* Ah, sasa nimeelewa! Ni kama mwanafunzi asiyesoma vizuri hawezi kufaulu mtihani.

**Mama Pendo:** Kabisa! **24. …….**. Umeielewa vyema.

**Neema:** Asante mama. Sasa naenda kufanya kazi zangu za shule.

**Mama Pendo:** Nenda mwanangu. Nakuombea mafanikio. **25. ……...**

**21.** A. Je
B. Kweli
C. Hapana
D. Baada

**22.** A. mapambo
B. rasilimali
C. hazina
D. vyombo

**23.** A. Anayepanda mbegu ovyo ovyo atapata mavuno mazuri.
B. Anayefanya mambo bila mpangilio hupata matokeo mabaya.
C. Anayepanda vizuri hulima vibaya.
D. Anayekula vibaya hupanda vizuri.

**24.** A. Vema
B. Mbaya
C. Hivyo
D. Nje

**25.** A. Usijali.
B. Kaza buti.
C. Endelea.
D. Piga moyo konde.

**Soma kifugu kifuatacho kisha chagua jibu kujaza nafasi 26 hadi 35**

Teknolojia ya kidijitali .....26. kubadilisha namna watu wanavyowasiliana. Simu mahiri, kompyuta, na intaneti .....27. watu kutuma ujumbe, kupiga simu au hata kufanya mikutano kwa video. Hali hii .....28..... mawasiliano kuwa ya haraka na rahisi, hata kwa watu walioko .....29. mbali.

Mitandao ya kijamii kama WhatsApp, Facebook, na X (zamani Twitter) .....30. mawasiliano ya papo kwa hapo. Hata hivyo, matumizi mabaya ya vifaa hivyo yanaweza .....31. changamoto kama uenezaji wa habari za uongo, uraibu na .....32. wa faragha.

Ni muhimu kutumia vifaa vya kidijitali kwa .....33. na kwa lengo sahihi. Elimu kuhusu matumizi salama ya teknolojia .....34..... kupewa kipaumbele. Hii itasaidia jamii kufaidika bila .....35..... madhara.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 26. A. imeweza | B. inachangia | C. imekuwa | D. inalazimisha |
| 27. A. hushirikisha | B. hufanya | C. huwezesha | D. huamua |

28. A. huchelewesha B. huboresha C. huathiri D. huharibu
29. A. mtaa B. nchi C. maeneo D. sehemu
30. A. huongeza B. huathiri C. hurahisisha D. huchunguza
31. A. kuleta B. kuzuia C. kusababisha D. kumaliza
32. A. upotevu B. uvujaji C. uimarishaji D. uboreshaji
33. A. nguvu B. tahadhari C. muda D. pesa
34. A. inapaswa B. inaweza C. haifai D. imeshindwa
35. A. kupunguza B. kujua C. kuepuka D. kupata

**Chagua jibu mwafaka katika Maswali 36 hadi 50**

36. Kanusha sentensi hii.
Angewatii wazazi angepata baraka zao.
A. Hakuwatii wazazi wala kupata baraka zao.
B. Asipowatii wazazi hatapata baraka zao.
C. Asingaliwatii wazazi asingalipata baraka zao.
D. Asingewatii wazazi asingepata baraka zao.

37. Mtu akikwambia ‘karibu tule’ nawe utamjibu,
A. sawa B. ahsante
C. hewala D. starehe.

38. Chagua nomino zilizo katika ngeli ya U-YA.
A. ugomvi, uyoga.
B. uti, ubongo.
C. ulezi, ugonjwa.
D. ubele, ufito.

39. Msemo upi una maana ya kupata maendeleo mazuri?
A. Kujikaza kisabuni.
B. Kupiga hatua.
C. Kuenda shoti.
D. Kuenda segemnege.

40. Badili katika usemi wa taarifa.
“Wageni wetu watawasili kesho,” baba alisema.
A. Baba amesema kuwa wagemi wetu wangewasili kesho.
B. Baba angesema kuwa wageni wetu watawasili kesho.
C. Baba anasema kuwa wageni wetu watawasili siku ifuatayo.
D. Baba alisema kuwa wageni wetu wangewasili siku ambayo ingefuata.

41. Andika katika kauli ya kutendwa.
Dada alikivunja chungu cha mama.
A. Mama alivunjiwa chungu na dada.
B. Chungu kilivunjiwa mama na dada.
C. Chungu cha mama kilivunjwa na dada.
D. Dada alimvunjia mama chungu chake.

42. Chagua maelezo yaliyo sahihi.
A. Tathlitha ni shairi lenye beti tatu.
B. Tathnia ni kipande cha pili cha mshororo.
C. Tarbia ni shairi lenye mishororo minne katika ubeti.
D. Mizani ni silabi zinazofanana katika ubeti.

43. Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
A. Wanafunzi wangu -hasa wa kike- wanalipenda somo la Kiswahili.
B. Mama, alipofika alituletea; matunda na mboga.
C. Kumbe, yeye ndiye aliyekusaidia?
D. Je? Ukikimbizwa na simba utafanya nini!

44. Tambua maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo:
Magari yote yalikwama barabarani.
A. Kiwakilishi, nomino.
B. Kivumishi, kiwakilishi.
C. Kivumishi, kielezi.
D. Nomino, kielezi.

45. Ni jawabu lipi linaloonyesha nomino za aina moja pekee?
A. Moshi, wito, uovu.
B. Viatu, nywele, maziwa.
C. Kusoma, kuimba, kusudi.
D. Maisha, maji, maua.

46. Tambua kivumishi katika sentensi ifuatayo.
Mkeka mpya umeuzwa tena bila idhini.
A. tena
B. idhini
C. mpya
D. bila

47. Kisawe cha ‘ajuza’ ni
A. mjukuu
B. shaibu
C. nyanya
D. bikizee.

48. Chagua maelezo sahihi.
A. Nukta pacha hutumiwa kabla ya kutaja mifano ya vitu.
B. Mabano hutumiwa kunukuu maneno ya usemi halisi.
C. Koloni hutumiwa baada ya kutoa orodha.
D. Koma hutumiwa katikati ya kila sentensi.

49. Ni sentensi ipi isiyoonyesha kauli ya kutendeka?
A. Maji yalimwagika usiku kucha.
B. Mgonjwa ametapika baada ya kumeza

dawa.
C. Wengi wamesikika wakikemea ufisadi.
D. Chakula chake kinalika.

50. Andika wingi wa sentensi hii.
Ufagio ulinunuliwa sokoni.
A. fagio zilinunuliwa sokoni.
B. Ufagio zilinunuliwa sokoni.
C. Fagio zilinunuliwa masokoni.
D. Ufagio ulinunuliwa masokoni.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

**MAJIBU**

1. C
2. C
3. B
4. B
5. C
6. B
7. C
8. C
9. D
10. C
11. A
12. B
13. A
14. B
15. A
16. B
17. B

18. B
19. B
20. D
21. A
22. C
23. B
24. A
25. B
26. A
27. C
28. B
29. C
30. C
31. A
32. B
33. B
34. A
35. D
36. D
37. B
38. C
39. B
40. D
41. C
42. C
43. C
44. B
45. D
46. C
47. D
48. A
49. B
50. C